Wapendwa Mapadre, Watawa na Waamini Walei **13.02.2012.**

Jimbo Katoliki Moshi.

**Kristo! Tumaini letu.**

**YAH: KUTEGEMEZA KANISA.**

**UTANGULIZI.**

Tarehe **11 Februari 2012** ilikuwa siku ya ripoti ya mapato na matumizi ya Ofisi Kuu ya Jimbo na bajeti yake. Yafuatayo ni maelezo muhimu na ya msingi ya kutusaidia kujenga utamaduni wa maendeleo tukiwa na ufahamu na uelewa sahihi kama familia ya Mungu yenye kuongozwa na neno la Mungu na malezi ya Kanisa lake. Ujumbe huu unaletwa kwenu ili uchokoze majadiliano na kuhamasisha moyo wa uwajibikaji na ushirikiano katika Kristo kwenye taasisi zetu hususan familia, JNNK, vigango, parokia, jimbo, taifa na hata Kanisa Ulimwengu. Ujumbe huu urudiwe mara kwa mara mpaka ueleweke vyema.

**KANISA LA KWANZA.**

Jumuiya ya wakristo wa kwanza ilikuwa moyo mmoja na roho moja wakishirikishana mali zao kwa uhitaji wa kila mtu. Hata wengine waliuza mashamba yao na kuwakabidhi mitume kwa matumizi ya pamoja **Mate.4:32-37.** Waliodanganya kama Anania na mkewe Safira waliangamia **Mate.5:1-11.**

Jumuiya-Kanisa zilivyoongezeka hali ilibadilika. Yerusalemu ilikuwa makao makuu. Jumuiya za waamini zilipeleka michango Yerusalemu. “Maana makanisa ya Makedonia na Akaya yameamua kutoa mchango wao kuwasaidia watu wa Mungu walio maskini huko Yerusalemu. Wao wenyewe wameamua kufanya hivyo; lakini, kwa kweli, hilo ni jukumu lao kwa hao” **Rom. 15:26-27.** Naye Paulo aliwahimiza Wagalatia kuhusu mchango huo:” Kila Jumapili kila mmoja wenu atenge kiasi cha fedha kadiri ya mapato yake, ili …wale mtakaowachagua miongoni mwenu wapeleke barua na zawadi zenu Yerusalemu” **IKor.16:1-3.**

Makanisa mbalimbali walipeleka michango ya ukarimu Yerusalemu kwa lengo la kufanikisha shughuli za uchungaji na ufadhili wa Kanisa. Ndivyo waamini walivyoshiriki taabu za Kanisa kwa sadaka na ukarimu wao. Paulo mtume aliwashukuru na kuwabariki Wafilipi kwa upendo walioonesha katika utoaji kwa wenye shida. Alieleza zawadi zao “kama dhabihu yenye harufu nzuri, tambiko inayokubaliwa na kumpendeza Mungu. Basi, Mungu wangu, kwa utajiri wake mkuu kwa njia yake Kristo, atawapeni mahitaji yenu yote” **Fil.4:14-19.** Utoaji wa namna hii ni kama mtu kununua hisa kwa Mungu. Faida na Baraka zake ni magawio mengi kupita hata ufahamu wetu.

**KANISA LA MISIONI.**

Wamisionari walipotuletea Injili hali yetu ilionekana kuwa duni kiuchumi, kiafya na kielimu. Kwa lengo la kutuletea mapinduzi ya haraka walijitosa kutafuta misaada ya kujenga mashule, vituo vya afya na makanisa. Tangu mwanzo tulikaa mkao wa kupokea misaada na wao wakawa kwenye mtazamo kwamba bila wao hatuwezi! Huo ukawa namna ya utamaduni ulioota mizizi siku hadi siku. Makanisa ya Ulaya na Marekani walijinyima ili sisi tujengewe makanisa, mashule na hospitali. Familia na marafiki wa baadhi ya wamisionari walijitolea kwa ziada ili watoto wao wafanikishe miradi mbalimbali hapa Jimboni kwetu. Tunawashukuru kwa jitihada zao na Mwenyezi Mungu awabariki sana. Haikuwa rahisi kwao kutusaidia. Walihangaika wakafanikisha. Tunatakiwa tutafakari utamu wa misaada unavyoweza kutulemaza kifikra. Hata asali ikiliwa nyingi mno hudhuru tumbo. Dhana kwamba hatuwezi kufanikisha wenyewe bila wafadhili ni ya hatari sana kwa maendeleo. Mpaka leo wapo waamini wanaosadiki kwamba Kanisa – Parokia, Jimbo lina mali nyingi kiasi kwamba halihitaji kutegemezwa na waamini. Wenye mawazo kama hayo ni waregevu wa maendeleo ya Kanisa kwani hawana moyo wa ushiriki. Watapenda Kanisa lifanikishe mipango mizuri bila ushirikiano wao wa dhati. Hizo ni fikra potofu. Wamisionari waliweka misingi ya Imani na Maendeleo hapa Jimboni jinsi kitabu cha Mwondoko kinavyoeleza. Tangu mwaka **1953** tumekuwa Jimbo Katoliki Moshi. Kuwa Jimbo ni kupokea hadhi na wajibu wa kuwa Kanisa Mahalia lenye kujitegemea kiutawala, kiuchungaji, kiuchumi na kimisionari. Huu ni mwaka wa **59** wa kuwa Jimbo. Tangu Wamisionari watuachie Jimbo tumepiga hatua nyingi katika kuendeleza na kuongeza huduma za elimu, afya na uinjilishaji. Tumshukuru Mungu kwa kutuwezesha. Upo mwamko mzuri sana kwa Mapadre na waamini wanavyowajibika na kushirikiana kuleta maendeleo katika vigango na parokia kwa michango yao ya mawazo na mali. Wapo wachache waaminio kwamba wafadhili ndio watakaotuletea maendeleo. Ukweli ni kwamba sisi sio tena kanisa la kimisioni bali ni kanisa mahalia kwa miaka **59.** Yatupasa tujitegemee kama Kanisa kifikra na kiutekelezaji. Tutumie sana Mwondoko na Mpango Mkakati wa Jimbo katika roho ya Mtaguso wa II wa Vatikano.

**KANISA MAHALIA**.

**Mkristo ni kiungo muhimu cha Kanisa**.

Kwa kuwa utajiri wa Kanisa ni waamini, ni muhimu sana kila mkristo ajitambue kuwa kiungo cha Mwili wa Fumbo wa Kristo. Kwa ubatizo tumefanywa kuwa mwili mmoja yaani Kanisa na Kristo ndiye kichwa cha mwili huo. Tu viungo vingi muhimu vya mwili mmoja **IKor. 12:12-30.** Uwajibikaji, heshima na kutambua umuhimu wa kila kiungo ni mambo ya msingi yatakiwayo yaeleweke kwa watoto na watu wazima. Udhaifu wa kiungo kimoja ni hasara kwa mwili wote na ufanisi wa kiungo chochote ni furaha na heri kwa mwili wote hususan familia, JNNK, kigango, Parokia hata Jimbo. Mkristo ajitambue kuwa kiungo hai kwa kuyatii maagizo ya kichwa; kiungo hakijiongozi chenyewe. Mkristo aone fahari kuwa mwanakanisa hai anayejali wokovu na maendeleo yake binafsi na ya pamoja. Uhai wa imani huonekana wazi katika matendo ya mtu.

**Heshima ya kiumbe ni kumwabudu Mungu na kumtolea sadaka.**

Sisi ni viumbe, yatupasa tumwabudu Mungu mwumba wetu (Amri ya kwanza ya Mungu). Mtume Paulo anauliza: “Una kitu gani wewe ambacho hukupewa?” **IKor.4:7.** Uhai, ukombozi na wito wa kumjua, kumpenda na kumtii Mungu ni zawadi za msingi tulizopewa na Mungu bila hata kustahili. Maisha yana faida gani yasipotukuza zawadi hizo tatu? Tuwe watu wa shukrani kwa Mungu. Tujisikie kuwa wadeni wa Mungu. Tufanye kila liwezekanalo ili imani yetu ionekane wazi katika matendo. “Imani bila matendo imekufa” asema Mtume Yakobo **Yak.2:26.** Mara nyingi twadhani tunayo haki ya kuishi na kupata kila kitu tupendavyo hata kwa njia ya dhambi. Tunadhani fikra zetu zatosha kupangilia mbinu za mafanikio. Mzaburi asema: “Hakika binadamu hawezi kujikomboa mwenyewe; hawezi kumlipa Mungu gharama ya maisha yake, maana fidia ya maisha ni kubwa mno. Hawezi kutoa kitu chochote kinachotosha, kimwezeshe aendelee kuishi asipate kuonja kaburi” **Zab.49:7-9.** Katika sadaka ya Misa, Yesu hujitoa kwa Baba kwa ajili ya wazima na wafu. Waamini hutoa mchango na vipaji kwa ajili ya kushiriki gharama za madhabahu yaani vifaa vya ibada hasa mkate na divai. Kwa hiyo kushiriki Misa ni pamoja na kupokea neno, kutoa mchango na vipaji na kupokea Komunyo Takatifu. Kutoa kilichoandaliwa ni wajibu na heshima kwa Mungu. Yesu aliisifia sadaka ya mjane maskini kwa kuwa alitoa kwa ukarimu tegemeo la maisha yake **Luka 21:4.** Mara ngapi watu hutupa mabaki na masazo kwenye chombo cha sadaka! Sadaka yatakiwa iandaliwe kwa dhamira ya kumshukuru Mungu kwa ukarimu wake. Kwa hiyo mchango-misa utolewe kwa ufahamu na unyenyekevu kwani hiyo ni sala ya shukrani inayotuunganisha na sadaka ya Yesu altareni. Hatuwezi kamwe kutoa kama Mungu atoavyo kwetu! Kwa hiyo tuwe na mawazo chanya kuhusu michango na zaka.

Tukumbuke kila tulicho nacho tumepata kutoka kwa Mungu; tumshukuru kwa kumrudishia asilimia **10** na kubaki na asilimia **90** kwa shughuli za maisha anayotupa. Kwa kulipa zaka na shukrani mazao unatimiza wajibu wa kumshukuru Mungu na kuitimiza amri ya **5** ya Kanisa: “Saidia Kanisa Katoliki kwa zaka” pamoja na gharama nyingine za dini. Utoaji kwa ukarimu umeanzia kwa Mungu na ni fadhila yao wampendao Mungu.

**Zaka ni wajibu na shukrani kwa Mungu.**

Chimbuko la Zaka ni Babu yetu wa imani Ibrahimu alipotoka vitani na ushindi: “Naye Melkisedeki mfalme wa mji wa Salemu, ambaye alikuwa kuhani wa Mungu mkuu, akaleta mkate na divai, akambariki Ibrahimu na kumtukuza Mungu aliyempa ushindi. Ndipo Ibrahimu akampa Melkisedeki mchango wake sehemu ya kumi ya vitu vyote alivyokuwa navyo” **Mwa.14:17-20.** Kwa mtu wa imani, fanaka ni baraka na kushukuru ni wajibu; na mwenye kushukuru hubarikiwa zaidi. Waisraeli waliendeleza tendo hilo kama desturi bora ya kukiri ukarimu wa Mungu na wajibu wa kutoa shukrani. “Toeni zaka ya mazao yenu yote ya shambani kila mwaka” **Kumb.14:22.** “Zaka za mazao…yote ni mali ya Mwenyezi Mungu, ni takatifu kwa Mwenyezi Mungu” **Law.27:30.** Nabii Malaki aliwaasa Waisraeli wamrudie Mungu kwa kuwajibika kwa swala la zaka. “Mnanidanganya kuhusu zaka na dhabihu zenu. Nyinyi na taifa lenu lote mmelaaniwa kwa sababu ya kunidanganya. Leteni ghalani mwangu zaka yote,

ili nyumbani mwangu kuwe na chakula cha kutosha” **Mal.3:8-9.** Hata Yesu na mtume Petro walilipa zaka kwa ajili ya hekalu **Mt.17:24-27.** Kwa kulipa zaka mkristo anathibitisha imani yake kwa Mungu na Kanisa lake. Kila mkristo aliyefikia umri wa miaka **18** na kuendelea anao wajibu wa kulipa zaka. Hata kama hajapokea Komunio na Kipaimara, mkristo mwenye miaka**18** na kuendelea anao wajibu wa kulipa zaka. Zaka ni asilimia kumi ya pato la mtu kwa mwaka ambalo anapaswa kulitoa kwa Kanisa. Tuachane na dhana kwamba asilimia **90** ni ndogo kuliko asilimia **10.** Tumpe Mungu yake Mungu na mengine yatabarikiwa.

Kanisa mahalia linakuwa na nguvu ya ustawi wakati waamini wanaelewa na kutimiza wajibu kwa moyo wa sadaka, imani na furaha; sio kwa huzuni, manung’uniko na malalamiko. Katika maisha ya kawaida ipo michango ya sherehe, misiba, na mingi ya kuondoa shida mbalimbali katika jamii. Michango kwa ajili ya shughuli za kiroho ni michango halali na ni sehemu muhimu ya kushuhudia imani kwa matendo. Michango iliyopelekwa Misioni ilitokana na ukarimu wa wakristo waliowajibika kwa utoaji. Wao walitoa nasi tukapokea. Ni wajibu wetu tutoe kwa ukarimu kwa ajili ya Kanisa lote la Mungu. Kutolipa zaka ni dhambi kubwa ya kumwibia Mungu na Kanisa. Dawa pekee ya dhambi ya wizi ni kurudisha, kutubu, kuungama, kuondolewa na kufanya kitubio. Nabii Malaki anasema “Kumdanganya Mungu ni kujitafutia laana”. Hakika tunahitaji Baraka sio laana za Mungu. Neno la Mungu lituongoze katika njia zake na sio fikra na hisia zetu.

**MAJUKUMU MATATU MAKUU YA KANISA MAHALIA KIUCHUMI.**

1.Kugharimia Majengo na Vifaa vya Ibada ya Liturjia: Kanisa, viti kanisani, altare, mavazi, vyombo vya ibada kama kalisi, mishumaa, chetezo, ubani na usafi wa kawaida pamoja na ukarabati wa makanisa ni wajibu wa waamini wa kanisa mahalia.

2.Kuwakimu wahudumu yaani Mapadre, Watawa, Waseminaristi wakubwa na Makatekista. Hawa ni wahudumu wa neno wenye kufundisha na kuhubiri. “Ole wao wasipohubiri!” **IKor.9:16-18.** Wanapowajibika hivyo wanapaswa kutunzwa na Kanisa yaani waamini **( Mf.Bima ya afya).** Ndivyo viungo vyashiriki taabu na faraja vya viungo vingine. Sio vyema wahudumu wa neno watangetange au kuhangaika kwa kukosa mahitaji ya maisha “maana mfanyakazi anastahili mshahara wake” **Lk.10:7.** Mwenye kuwategemeza hao wahudumu wa neno, huwa anashiriki wajibu na baraka zao moja kwa moja.

3.Mmoja ya wajibu wa Kanisa mahalia ni kuwa karibu na maskini kwa lengo la kuwasaidia kwa kuyanyanyua maisha yao na kuwahubiria habari njema ya ufalme wa Mungu. Yesu anatuambia: “Maskini mnao daima pamoja nanyi “**(Mt.26:11.)** “Kila kitu mlichomtendea mmojawapo wa hawa ndugu zangu wadogo, mlinitendea mimi”**(Mt.25:40).** Kwa kuwajali wenye shida twaonesha tunavyomjali Yesu anayetujia katika nafsi zao. Waamini wanatakiwa wawezeshe Kanisa kutoa msaada

kwa maskini yaani wahitaji kama yatima, wajane, wazee na wagonjwa wasiokuwa na msaada mwingine. Tangu mwanzo waamini waliwezesha Kanisa kutimiza majukumu yake.

Kwa hekima yake Mama Kanisa ameagiza katika kanuni zake: "Waamini wakristo hawana budi kusaidia Kanisa katika mahitaji yake ili liweze kuwa na kila linachohitaji kwa ibada takatifu, kwa kazi za kitume na ufadhili na kwa ajili ya matunzo yanayofaa ya watumishi" "Hawana budi pia kukuza haki ya jamii, na wakizingatia amri ya Bwana, kuwasaidia maskini kutoka katika mali zao" **MSK 222-(1+2).** "Waamini wakristo inawabidi kuutunza muungano wao na Kanisa muda wote hata katika matendo yao ya nje" "Wanapaswa kutimiza kwa uangalifu mkubwa wajibu zao kwa Kanisa zima na kwa kanisa lao mahalia kwa misingi ya sheria" **MSK 209-(1+2).** Kanuni mbili zilizotajwa zitupatie ari ya kujipanga vyema tuweze kujenga jimbo kwa bidii zaidi.

**TUFANYE NINI SASA?**

Maelezo yaliyotolewa yatusaidie mambo yafuatayo:

1. Tutambue kwa undani wajibu wa kutegemeza taasisi: kanisa la familia, kigango, parokia na jimbo. Mikono ya kanisa ni waamini wake wanaowajibika
2. Tuondokane na dhana na fikra potofu kuhusu utoaji wa michango ya kanisa, mchango-misa na zaka. Michango ya kanisani isitafsiriwe kuwa kero.
3. Tuimarishe uwajibikaji wa bahasha ya JNNK kwa askofu kwa ajili ya kufanikisha majukumu ya Jimbo.Wasioshiriki wajiulize wana ushirika gani na wanajimbo wenzao.
4. Kila Parokia na Kigango teule kichangie mfuko wa Jimbo asilimia **20** ya mapato ya zaka na shukrani mazao kwa pamoja. Jimbo huwezeshwa na taasisi zake kwa kiwango cha kueleweka ili lifanikishe shughuli kubwa k.v. **Kujenga** ***Tawi la Benki ya Mkombozi hapa Moshi.***
5. Benki ya Mkombozi ni ya Kanisa Katoliki kitaifa. **Tutaimarisha nguvu ya umiliki huo kwa waamini wengi kununua hisa za Parokia, Vigango, Mashirika na Vyama vya kitume, JNNK, Shule, Hospitali, Mashirika ya kitawa na hata watu binafsi.** Maaskofu wametoa nafasi hii ya upendeleo wa kununua hisa hizo kwa wakatoliki kabla ya kuzitoa kwa umma. Benki ya Mkombozi inasubiri kukaribishwa majimboni. Tafadhali tutumie fursa hii tuwekeze kwa ari mpya katika biashara yenye tija katika ulimwengu wa leo. Ushiriki wako ni muhimu sana kwa ufanisi wa mradi huu.
6. Kila taasisi ya Kanisa ihakikishe inadhibiti mapato na matumizi yake na kuwa na ripoti sahihi iliyohakikiwa kitaalam. Bajeti iwe ndiyo dira ya kuendesha taasisi zetu na kamati za mipango, fedha na maendeleo zishirikiane na mapadre vizuri.
7. Kuanzia mwakani tutafuata utaratibu ufuatao kwa siku za bajeti.
   Bajeti ya Parokiani na Vigango teule ni Jumapili ya tatu Januari **(20.01.2013).**
   Jumamosi ifuatayo **(26.01.2013)** Tutakuwa na Misa ya Shukrani Mazao Jimbo. Siku hiyo, Paroko na Padre Kiongozi pamoja na Mhazini walete Jimboni kimaandishi:
   1.Ripoti ya fedha na bajeti iliyosomwa Jumapili; 2.Ripoti ya Michango ya mwaka uliopita; 3.Ripoti ya Bahasha ya JNNK kwa Askofu ya mwaka uliopita na 4. Asilimia 20 ya zaka na mazao ya mwaka

uliopita iliyowekwa kwenye akaunti ya Jimbo (risiti ya benki). Msarifu Mkuu ataandaa fomu maalum za kutoa ripoti hizo kwa urahisi.
Bajeti ya Jimbo itasomwa Jumamosi ya pili ya Februari **(9.02.2013).** Bajeti zinapoandaliwa ni muhimu malengo ya mwaka yawekwe wazi ili yafanyiwe kazi, na baadaye tathmini. N.B.Tuanze utamaduni wa kuweka **10%** ya kila pato kwa dharura.
**TAMATI.**

Wapendwa Katika Kristo,
Natumia nafasi hii adimu kueleza shukrani zangu kwa Mwenyezi Mungu kwa Baraka na usalama anazotujalia katika familia na taasisi zetu hapa Jimboni. Aidha nashukuru kwa mafanikio yanayoonekana katika parokia na vigango kutokana na roho ya kuwajibika na kushirikiana katika Kristo. Dira yetu yasema**: "Jimbo Katoliki la Moshi likiongozwa na tunu za Injili linatazamia kuwa familia ya Mungu iliyo na mshikamano na majitoleo yenye maisha bora kiroho na kijamii".** Tuimarishe mshikamano na majitoleo kwani hiyo ndiyo njia ya kuwa familia. Utume umeelezwa: **"Jimbo Katoliki la Moshi linajitosa/linajituma kujenga familia ya Mungu yenye umoja, Mshikamano na Uwajibikaji kwa kushuhudia na kutangaza Habari Njema ya Injili, kwa kufundisha na kutoa huduma za kijamii kwa uungwana/utu wema, majitoleo na uwazi".** Ninawapongeza Mapadre, Watawa na Walei waliojitosa kwa ziada katika kutekeleza mipango ya kimapinduzi katika uchungaji na maendeleo ya Jimbo letu. Mafanikio yaliyopatikana yatupatie moyo wa kufuatilia mipango yetu kwa umakini zaidi ili mwaka kesho tufanye tathmini na kujipanga kwa hatua nyingine. Ninawapongeza viongozi wa ngazi zote kwa jinsi wanavyowajibika. Aidha viongozi waregevu wajirekebishe, la sivyo wachaguliwe wengine walio tayari kuhudumia Kanisa. Ninawapongeza waamini walei kwa michango yao mbalimbali kwa ajili ya Parokia, Jimbo, Taifa na hata Kanisa Kiulimwengu. Mwenyezi Mungu awazidishie kwa ukarimu wenu.
Tunazindua leo sala maalum ya kuombea familia zetu. Sala hii itasaliwa katika makanisa na taasisi za kanisa hapa Jimboni kuanzia kesho. Kuanzia sasa mpaka **Oktoba 22** mwaka huu tutapata mafundisho ya kuimarisha familia zetu. Familia ndiyo taasisi ya msingi na shule ya awali ya upendo na imani. Uimara wa familia ndio msingi bora wa taifa, na ubovu katika familia ni unyonge na kifo cha jamii na taifa. Wakati Kanisa Katoliki litakutanisha Familia nyingi huko Milano Roma mwezi Mei, sisi tutakuwa tunajadili namna ya kuimarisha na kufurahia zawadi ya familia Mwenyezi Mungu aliyopenda tuzaliwe, tutunzwe kiimani na kijamii ili tukue na kukomaa kiutu na kitakatifu. Nawaomba Mapadre wasimamie swala hili kikamilifu na kwa ushirikiano katika ngazi za Vikarieti. Tuziimarishe familia zetu kwa sala na malezi.

**NAWATAKIENI BARAKA NA AMANI TELE KUTOKA KWA BWANA WETU YESU KRISTO.**

**Wenu Katika Kristo,**

**+ Isaac Amani.**